hakielimu

enabling citizens to make a difference in education and democracy

# Serikali Ipitie Upya Sheria, Kanuni na Miongozo Kufuta Vipengele Vinavyo Ruhusu Matumizi ya Adhabu ya Viboko Shuleni

**Ndugu waandishi wa Habari**

Tumepokea kwa masikitiko taarifa ya tukio la adhabu ya kikatili waliyoipata mwanafunzi wawili wa shule ya msingi Kakanja iliyopo wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera. Tukio hili lilitekelezwa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo Isaya Benjamini ambaye anaonekana kwenye kipande kifupi cha video akiwacharaza bakora kwenye nyayo za miguu wanafunzi wawili. Tunaamini kitendo hiki kinakiuka sio tu haki za watoto bali pia ni kinyume na maadili ya kazi ya ualimu na malezi bora ya wanafunzi.

Tunaipongeza Serikali kupitia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mh. Prof. Adolf Mkenda na uongozi wa mkoa wa Kagera kwa kuchukua hatua za haraka na za awali dhidi ya mwalimu aliyehusika na ukatili huo; ikiwa ni pamoja na kumvua nafasi yake ya Ualimu Mkuu, kumsimamisha kazi na kuunda tume ya kuchunguza tukio hilo ili hatua za kisheria ziweze kufuata. Katika taarifa yake iliyorushwa na kunukuliwa katika vyombo mbalimbali vya habari, Waziri Mkenda anasema '*Nimeona hii 'clip' inazunguka sana mitandaoni, tumekwisha fuatilia, Mwalimu ameshasimamishwa kazi na uchunguzi unaendelea na hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yake; sasahivi hayuko kazini*''.

Tukio hilo ambalo pia limekemewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu Mh. Dkt. Doroth Gwajima; ni sehemu ya matukio mengi ya unyanyasaji na ukatili kwa watoto shuleni ambayo yanaendelea kuongezeka. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Ukatili nchini iliyotolewa na Jeshi la polisi, visa vya ukatili kwa watoto viliongezeka kwa asilimia 25.9% kutoka visa 5,803 vilivyoripotiwa Mwaka 2015 hadi visa 7,388 Mwaka 2020.

Mwaka 2016 katika shule ya Sekondari ya Kutwa huko Mbeya; walimu watatu kwa pamoja waliripotiwa kumpa adhabu ya viboko na ngumi mwanafunzi na kusababisha kulazwa hospitali; mwaka 2018 mwanafunzi Sperius Eradius wa Shule ya Msingi Kibeta, Manispaa ya Bukoba Mkoani Kagera alifariki kutokana na adhabu ya viboko kutoka kwa mwalimu wake. Hii ni mifano ya matukio ya ukatili shuleni ambayo yanashabihiana na hili na yameripotiwa katika vyombo vya habari kwa nyakati tofauti.

Katika utafiti uliofanywa na Shirika la HakiElimu Mwaka 2020; takribani 87.9% ya watoto wa shule waliripoti kufanyiwa ukatili wa kimwili huku asilimia 90% kati ya hao walisema ukatili wa kimwili waliofanyiwa ulitokana na adhabu za viboko zinazotolewa shuleni. Katika utafiti huu, asilimia 54.9% ya watoto walisema walimu wao na walezi wanatumia kupiga ngumi na makofi kama sehemu ya adhabu.

**Ndugu wana habari**

Tanzania bado inakumbatia adhabu ya viboko kwa watoto na shuleni. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Elimu (Juu ya Adhabu za Viboko) wa Mwaka 2002 (The Education Corporal Punishment Regulations, 2002), Mwalimu Mkuu anaruhusiwa kutoa adhabu ya viboko kwa wanafunzi au kukasimisha jukumu hilo kwa mwalimu mwingine. Mwongozo huu unapewa nguvu na Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 (na

Registration
00NGO/R2/000066
*Board of Directors*
Richard Mabala
Mwajabu Possi
Sylvester Orao
Helen Kijo-Bisimba
Ilumninata Tukai
Victoria Lihiru
John Kalage

739 Mathuradas Road • P.O. Box 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Telephone: (255 22) 2151852 or 3 • Cell: (255) 754 354 681 • Fax: (255 22) 2152449 • Email: info@hakielimu.org • Website: www.hakielimu.org

mabadiliko ya 2002) ambayo chini ya kipengele cha 60 kinaruhusu utolewaji wa adhabu mbalimbali kama sehemu ya kuhimiza nidhamu kwa watoto. Pamoja na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 (Tanzania Bara) kuzuia vitendo vya kutesa au vya kikatili kwa mtoto; hata sheria hii haitoi katazo la moja kwa moja la adhabu ya viboko kwa watoto.

Pamoja na kuwa madhara ya adhabu yameelezwa vizuri kwenye mafunzo ya taaluma ya ualimu ikiwemo maumivu ya aina mbalimbali kwa mtoto, kujenga chuki na hata kupunguza motisha ya kujifunza au kwenda shule; bado sehemu kubwa ya walimu wetu wanaona matumizi ya viboko ndio njia rahisi na yenye ufanisi kuhakikisha nidhamu shuleni na kuhimiza watoto kujifunza kwa bidi.

Walimu wanasisitizwa kutumia mbinu mbadala katika kusimamia nidhamu ya wanafunzi. Kwa mfano wanashauriwa kutumia vichocheo hasi ili kuwafanya wanafunzi wasiendelee na mienendo ambao haifai badala ya adhabu ikiwemo adhabu ya viboko. Hata hivyo, matumizi ya njia mbadala kusimamia nidhamu yanategemea sana uwezo wa walimu katika kuzitumia. Kinachojitokeza wazi ni kwamba walimu wengi wanashidwa kutumia njia mbadala na kwa sababu sheria na miongozo inaruhusu viboko basi wanachagua viboko badala ya vichocheo hasi.

Kutokana na matukio haya, HakiElimu tunatoa wito kwa serikali kuchukua hatua ambazo zitakomesha kabisa matumizi ya adhabu za viboko shuleni na kuhimiza adhabu chanya/adhabu mbadala ambazo sio za kikatili. Ni rai yetu vipengele vya Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978, Mwongozo wa Elimu Juu ya Adhabu za Viboko wa Mwaka 2002 na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009; vipitiwe upya ili kukataza kabisa matumizi ya viboko shuleni na kuzuia adhabu nyingine ambazo zinaweza kutoa mwanya wa ukatili kwa watoto kufanyika.

Sambamba na mapitio haya ya sheria na miongozo, HakiElimu pia tunapendekeza yafuatayo;-

- Programu ya uanzishwaji wa shule salama 600 nchi nzima ambayo inalenga kuondoa ukatili wa namna yoyote kwa watoto na kuzifanya shule kuwa mahali salama na rafiki pa kujifunzia ambayo imetangazwa hivi karibuni na serikali, ilenge shule zote 18,000 zikiwemo shule za msingi 12,000 na shule za sekondari 5000. Ni wito wetu kwa srikali kuwa program/mpango huu uingizwe katika miongozo na kanuni za uendeshaji wa shule ili utekelezwe kwa shule zote. Serikali inaweza kushirikiana na Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na jamii kufanikisha azma hii.
- Serikali iweke mipango endelevu ya kuimarisha mifumo rasmi ya ulinzi na usalama wa watoto shuleni ikiwa ni pamoja na kuharakisha uanzishwaji wa Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto shuleni (Child Protection Desks) pamoja na Mabaraza ya Watoto (Children Council).

- Serikali na wadau kuendelea kutoa elimu kwa wanafunzi, wazazi na jamii ili kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto wetu nyumbani, shuleni, nyumba za ibada na maeneo yote ambayo watoto hukusanyika .

- Serikali ichukue hatua kali dhidi ya wote watakaobainika kuhusika na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ili kukomesha vitendo hivyo ndani na nje ya shule.

- Mafunzo kazini ya walimu yanayoendelea kwa sasa yahusishe moduli inayohusu utoaji wa adhabu chanya na jinsi ya kuwarekebisha wanafunzi wenye matatizo ya kitabia.

- Mafunzo ya walimu tarajali yahusishe katika ngazi zote kozi ya maalumu ya jinsi ya kuwafundisha watoto wenye matatizo ya kitabia na utoaji wa adhabu chanya.

- Miiko na maadili ya walimu ihuishwe ili kuwagusa hata walimu ambao wanashindwa kuzuia matendo ya ukatili kwa watoto yanayofanywa na walimu wenzao. Katika matukio mengi tumeona watoto wakichapwa viboko huku walimu wengine wakishuhudia. Ni muhimu kuhimiza walimu waandamizi wenye uwezo watumike kuwasaidia walimu wengi kuimarisha stadi zao za maisha (life skills) na uwezo wa kukabiliana na changamoto za wanafunzi.

- Masomo yanayohusiana na maadili yafundishwe na walimu wenye uwezo ili kuwezesha wanafunzi kukuwa kimaadili na kiroho.

- Ushirikiano wa wazazi na walimu ni jambo ambalo linapaswa kupewa kipaumbele ikiwemo kuweka bayana kikanuni wajibu wa walimu kwa wazazi.

**Dkt. John Kalage**
**Mkurugenzi Mtendaji – HakiElimu**
**Dar es Salaam - 26 Januari 2023 -**